**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents MoF Budget

2018-11

# Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Katika Wizara ya Fedha na Mipango,2019-20

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/662

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

MU.01. Nov. 2018

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 94(5) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

NOVEMBA, 2018

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**wakati dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) ni Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu; tunaingia mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango huo, hali ya uchumi na maendeleo ya watu katika kaya zao hapa nchini ikiwa mbaya zaidi kuliko awamu zote nne za Serikali zilizotangulia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na William Attwell mwaka 2017 na kuchapishwa katika mtandao wa 'Fronteers Strategy Group'[1], ni kwamba; pamoja na ukuaji wa uchumi wa Tanzania unaotajwa kukua kwa kasi, na licha ya ongezeko la idadi ya watu kuwa kubwa; bado uwezo wa wananchi wa kununua bidhaa (spending/purchasing power) umebaki kuwa wa chini sana. Utafiti unaendelea kuonyesha kwamba, kutokana na kiwango kikubwa cha umasikini nchini Tanzania (ambacho kwa sasa kimefikia asilimia 47 ya idadi ya watu wote), jumla ya idadi ya wananchi(walaji) wenye uwezo wa kununua bidhaa,

---

[1]http://blog.frontierstrategygroup.com/2017/05/tanzaniasconsumers-overlooked-overestimated/

ni chini ya nusu ya ile ya Kenya licha ya nchi hiyo kuwa na idadi ndogo ya watu kuliko Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** utafiti huo unaonyesha pia kwamba; zaidi ya asilimia 70 ya watu wazima wanaofanya kazi hawana kipato cha uhakika. Aidha, kipato hichohicho kisicho cha uhakika, hukumbwa na dhoruba ya kupanda na kushuka kwa mwenendo wa uchumi mara kwa mara. Matokeo yake ni kwamba, watu walio wengi wana uwezo wa kununua mahitaji ya msingi tu ili kuweza kujikimu kimaisha. Kwa hiyo, ni sehemu ndogo tu ya watu wenye kipato cha ziada cha kuweza kununua bidhaa kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo ni kwamba; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kutimiza dhima yake ya kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu ikiwa huu ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango huo ambapo wananchi walio wengi hawana uwezo wa kununua bidhaa kwa ajili ya maendeleo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni muujiza wowote unaoweza kufanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliobaki wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ili kuifanya asilimia 70 ya watanzania wasio na kipato cha uhakika kuwa nacho. Aidha, hakuna uhakika kama kwa kipindi cha mwaka mmoja uliobaki tunaweza kufuta kiwango cha umasikini cha asilimia 47 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya watu wenye kipato cha kati kama Serikali hii ya awamu ya tano inavyojinasibu.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa ya Mpango kushindwa kuifikia dhima yake ni kitendo cha Serikali kuitenga Sekta Binafsi katika mchakato mzima wa uendeshaji wa uchumi wa Nchi. Mpango umeeleza vizuri kuwa miradi yote ambayo ni ya kibiashara iachwe itekelezwe na Sekta Binafsi isipokuwa kama kuna sababu nzito ya kufanya vinginevyo ***"commercially viable projects should be left to the private sector, unless there is strong justification for doing otherwise"***[2]. Lakini Serikali imeamuza kukiuka mwongozo wa Mpango ulioidhinishwa na Bunge na kung'ang'ania kutekeleza

[2] National Five Year Development Plan 2016/17 – 2020/21 p.90

miradi yote yenyewe bila kuishirikisha Sekta Binafsi. Miradi hiyo ni kama vile Mradi wa ujenzi wa Reli ya Standard Gauge, Liganga Mchuchuma Industrial Park, Mtwara Petrochemical Special Economic Zone na Bagamoyo Special Economic Zone.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, ili uchumi uwe shirikishi na miradi ya maendeleo iweze kutekelezwa kikamilifu na kuwanufaisha wananchi lazima Serikali iachane na ukiritimba na ubinafsi na kuipa sekta binafsi nafasi katika ujenzi wa uchumi. Kitendo cha Serikali kung'ang'ania kufanya kila kitu yenyewe ni kuturudisha nyuma kwenye enzi za uchumi wa kijamaa ambao ulishashindwa tangu vita baridi imalizike.

## 2. KATIBA MPYA NA MUSTAKABALI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,** sote tunatambua kuwa Katiba ndio sheria mama. Katiba ndio taswira hasa ya taifa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na hata katika mambo mbalimbali ya utoaji wa huduma kwa wananchi. Katiba ndio msingi wa utoaji haki na wajibu wa kila raia. Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwa na

Katiba Mpya inayokidhi matakwa ya wananchi na inayoendana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na hata kutatua kero mbalimbali za kijamii serikali ya awamu ya Nne iliona ni vyema ikatoa fursa kwa wananchi kuleta maoni yao kuhusu aina ya Katiba wanayoitaka ili kuweza kunufaika kwa pamoja kama taifa.

**Mheshimiwa Spika,** hakuna uchumi bora wa nchi kama hakuna Katiba bora. Katiba ndio chombo pekee cha kulinda uhuru wa kila raia, ni chombo cha kuonyesha dira ya kule tunapotaka kuelekea na miiko yetu kama taifa. ***(Constitution is the only safeguard of our liberties; it is a solid expression of our vision and values as a nation).*** Kwa mantiki hiyo ***hatuwezi kamwe*** kuendelea kiuchumi kama hatuna katiba inayotoa taswira ya kule tunapotaka kwenda.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa matamanio ya kuwa na katiba mpya; serikali ilitumia mabilioni ya fedha ikiwa ni sawa na fedha za maendeleo za Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Maliasili na Utalii, Wizara ya Afya, Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017

pekee kama ilivyoainishwa kwenye fedha za maendeleo za Wizara mbalimbali kwenye kitabu cha Matumizi ya Maendeleo Juzuu ya Nne kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mabilioni hayo yaliyotumika serikali ilitumia muda mrefu wa takribani miezi mitatu ikijumuisha wajumbe zaidi ya 600 ambapo kila mjumbe alilipwa posho isiyopungua shilingi 300,000 kwa siku huku watendaji mbalimbali nao wakilipwa posho. Hii ikiwa na maana kwamba fedha za walipa kodi wa nchi hii ndizo zilizotumiwa na serikali ya CCM katika kutafuta Katiba mpya. Kwa umuhimu huo miradi ya huduma za kijamii kama maji, hospitali, madawa, nishati ya umeme ambapo huduma hizi muhimu kwa kila mwananchi hazikupewa kipambele kwa wakati huo kama mchakato wa Katiba Mpya.

**Mheshimiwa Spika,** kila raia wa nchi hii alitambua umuhimu wa kuwa na katiba mpya ambayo ilikuwa tegemeo la matumaini mapya ya kuwepo kwa utawala bora ambao ungechochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kujenga dhana ya uwajibikaji kwa kila raia na viongozi wao. Kinyume na mategemeo ya wananchi walio wengi mchakato wa upatikaji wa Katiba Mpya umekuwa na kiza kinene hasa katika serikali hii ya awamu wa Tano chini ya John Pombe Magufuli.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeweka misingi ya uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili ya Taifa kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 27 (1) na (2) na Ibara ya 28 (1) ya Katiba.

(1) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano,mali ya Mmlaka ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi ,na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine

(2) Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya Nchi nay a pamoja ,kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhiifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao.

28 (1) Kila raia ana wajibu wa kulinda,kuhifadhi na kudumisha uhuru,mamlaka,**ardhi** na umoja wa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwepo wa vifungu hivi katika Katiba ya Mwaka 1977 bado maliasili za nchi hii kama wanyamapori, misitu, madini, gesi, hewa, mafuta, maji na uvuvi, na hata mgawanyo wa ardhi umegubikwa na rushwa. Rasilimali zetu hususani madini na wanyapori

yamekosa usimamizi mzuri kiasi kwamba wachache ndio wanaonufaika na wananchi wetu hususani wale wanaozunguka maeneo hayo wamebaki kuwa maskini wa kutupwa. Vijiji vinavyozunguka misitu ya hifadhi na migodi imekuwa ikikumbwa na mapigano ya mara kwa mara,manyanyaso makubwa kutoka kwa baadhi ya wawekezaji na hata vifo kwa raia wema wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**mfano dhahiri nimauaji yaliyowahi kutokea katika mgodi wa Geita ambayo yamekuwa yakiripotiwa ikiwa ni pamoja na mauaji ya mwanafunzi wa darasa la tano katika shule ya Kivukoni marehemu Hoja Juma, vitendo vya mauaji, utesaji na kuwabambikizia kesi wanavijiji katika vijiji vinavyozunguka mgodi wa North Mara (NMGM), madhara ya kiafya pamoja na ucheleweshaji wa fidia katika maeneo mbalimbali ambayo serikali imewakaribisha wawekezaji bila kujali mustakabali wa wananchi katika maeneo hayo. Katika bonde la Loliondo wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiishi kama wakimbizi kutokana na manyanyaso makubwa wanayopata kutoka kwa baadhi ya wawekezaji wa kigeni huku serikali ikiyafumbia macho kutokana na rushwa kubwa kubwa zinazowanufaisha vigogo wa juu serikalini. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiipigia kelele kampuni ya Ortello Business

Corporation (OBC) kutoka falme za kiarabu ambae amekuwa mwiba mkubwa kwa wananchi wa Loliondo na kuona kama wametengwa katika taifa lao.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi kuhusu ushirikishwaji katika maamuzi yanayohusu utumiaji wa maliasili katika maeneo yao. Wananchi katika maeneo mbalimbali yenye rasilimali wamekuwa wakiyatunza vizuri na bila uharibifu wowote lakini pale wanapoanza kuletwa wawekezaji **bila kuwashirikisha na kinyume na matarajio yao** basi wananchi hao wamekuwa wakileta vurugu jambo ambalo sio afya kwa wawekezaji na haileti taswira nzuri katika sekta ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje. Mfano, vurugu zilizowahi kutokea Mwezi Januari na Februari mwaka 2013 mkoani Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwa kina sana katika hotuba ya nishati na madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuhusu katiba na mustakabali wa madini, mafuta na gesi asilia ikitoa mifano hai ya uzoefu wa nchi mbalimbali zilizofanikiwa baada ya kutatua changamoto mbalimbali za kikatiba, kisheria na kisera ili kulinda rasilimali za nchi. Mfano, nchi ya Norway imeweka mwongozo wa uwajibikaji katika matumizi ya maliasili kwenye Katiba yao Ibara ya 110 (b) ambapo ibara hiyo

inasema ***"every person has a right to an environment that is conducive to health and to natural surroundings whose productivity and diversity are preserved. Natural resources should be made use of on the basis of comprehensive long-term considerations whereby this right will be safeguarded for future generations as well"***. Mwaka 2009 nchi ya Bolivia ilianza mchakato wa kupata katika mpya ambao pamoja na mambo mengine katiba hiyo ililenga kuhakikisha kuwa mafuta na gesi asilia yanawanufaisha wananchi wa Bolivia.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi ni dhahiri katiba ya sasa ya mwaka 1977 haitaweza kutuhakikisha kuwa rasilimali zetu zinatukomboa katika lindi la umaskini ambao umetukabili kwa takribani miaka 56 sasa hata baada ya uhuru. Msimamo wa katiba pekee ndio utakaoweza kufafanuliwa vizuri katika sheria zetu zinazolinda rasilimali zetu. Mfano, katika Katiba ya Bolivia imeeleza bayana kuwa serikali ya nchi hiyo itakapoingia ubia na makampuni binafsi katika utafutaji na uvunaji wa mafuta na gesi asilia itakuwa na hisa zisizopungua asilimia hamsini na moja (51%) ya hisa zote. Jambo hili limewekwa bayana ndani ya katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mifano hii iliyo wazi ni kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa katika

usimamizi wa rasilimali zetu na ili kujikwamua katika hili tunahitaji maoni ya rasimu ya pili ya katiba ambayo ilipendekeza namna bora ya kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali zetu ili ziweze kumnufaisha kila mwananchi.

**Mheshimiwa Spika**, tulipofika sasa kama taifa hatuhitaji kuwa na katiba yenye viraka viraka. Tunahitaji kuwa na katiba mpya inayoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na ushindani wa kibiashara, mabadiliko ya kimfumo katika teknolojia, mashirikiano ya nchi mbalimbali na misimamo ya taifa na utaifa wetu, utawala bora, inayozingatia demokrasia , haki za binadamu na utawala wa sheria. Hivyo, rasimu ya pili ya katiba imetoa maoni ya wananchi ambayo kimsingi yanashabihiana na uhitaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** wananchi wanataka kuona katika ikiwashirikisha katika kumiliki faida zitokanazo na rasilimali zao ,ikiwa ni pamoja na michakato ya wazi ya utoaji wa leseni,katiba inayotoa mamlaka kwa Bunge kupitia na kuridhia mikataba mbalimbali inayohusu uvunaji wa maliasili ya Taifa ili kuongeza uwazi. Lakini pia, katiba itoe fursa kwa wananchi kuwa na sauti dhidi ya bunge lao, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapata taarifa ya kila

kinachoendelea ndani ya Bunge kwa kuwa Bunge ndio mkutano mkuu wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kurejesha mara moja mchakato wa rasimu ya pili ya katiba kwani katiba pendekezwa haikuzingatia maoni ya wananchi . Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutatua mkwamo wa mchakato wa katiba uliojitokeza katika serikali hii ya awamu ya tano bila sababu mahususi. Kuendelea kwa mkwamo huu kunatoa taswira hasi kwa serikali ya awamu ya tano sio tu ndani ya nchi bali pia katika medani za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu huu wa katiba mpya Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli kurejea katika Ibara ya kwanza ya Katiba ya Japan inayosema ***"The Emperor shall be the symbol of the State and of the unity of the People, deriving his position from the* will *of the* people *with whom resides sovereign power".***Ikiwa na maana kwamba Mheshimiwa Rais azingatie matakwa ya wananchi katika kuwaletea kile walichokiomba kwa muda mrefu ambacho ni rasimu ya pili ya Katiba.

### 2.1. Katiba Mpya ni Msingi wa Kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu

**Mheshimiwa Spika,** tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani imezuka desturi kuwatukuza viongozi wa umma na kufuata maelekezo yao katika utendaji wa Serikali na kuweka kando mifumo ya kitaasisi iliyopo kwa mujibu wa sheria jambo ambalo limekuwa kikwazo kikubwa katika kuifikia azma ya Taifa ya kuwa na maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na desturi hiyo mbaya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Serikali kukemea kasumba hiyo na badala yake kuweka katika ***"Kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu (Building Strong Institutions for Sustainable Development)"*** Sababu kubwa ya kuweka msisitizo huo ni kutokana na ukweli kwamba; ili kuwa na uendelevu (sustainability) katika jambo lolote ni lazima kuwe na mifumo imara ya kitaasisi, kanuni, taratibu na sheria zitakazofuatwa juu ya namna ya kutekeleza jambo hilo; na sio kufuata matakwa ya mtu au kikundi cha watu katika kufanya hivyo kwa kuwa watu ni wa kupita lakini taasisi na mifumo itabaki.

**Mheshimiwa Spika**, tunahitaji taasisi imara zinazozingatia misingi ya utoaji haki, ulinzi wa amani na zinazojali uwajibikaji

wa pamoja ili kujenga jamii jumuishi kwa maendeleo endelevu. Tunahitaji jamii ya watu huru wanaoishi bila hofu ya kutekwa, kutengwa na wapendwa wao, kuuawa, au vitisho vya namna yoyote. Tunahitaji kuwa na mahakama zilizo huru, zinazoweza kutoa maamuzi yanayozingatia sheria na haki bila mashinikizo ya mtu yoyote. Tunahitaji kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi inayofanya kazi kwa uhuru bila shinikizo la mtu au kikundi cha watu, tunahitaji kuwa na Bunge lenye uwezo wa kuikosoa serikali na kuiwajibisha serikali, tunahitaji jeshi la polisi linalozingatia sheria, usawa na haki za binadamu. Tunahitaji Jeshi la Wananchi lisiloegemea upande wowote,na linalowajibika kwa wananchi wote wa Tanzania na tunahitaji taasisi zote na idara za Serikali zifuate sheria na kanuni na sio maelekezo au matakwa ya viongozi.

**Mheshimiwa Spika**,ili taasisi nilizotaja ziweze kuwa imara ni lazima tuwe na Katiba Bora itakayoweka utaratibu wa jinsi taasisi hizo zinapaswa kuendeshwa. Aidha, katika kujenga taasisi imara tunahitaji kuwa na viongozi wanaoheshimu katiba na sheria za nchi. Katika ulimwengu wa sasa, hatuhitaji kumjenga mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu kwa kuwa hao watapita ila taasisi zitabaki. Katika historia; mifumo ya nchi iliyomjenga mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu imesambaratika,na kuziacha nchi hizo katika migogoro mikubwa na udikteta wa kutisha.

**Mheshimiwa Spika,**ni bahati mbaya sana kwamba taasisi tulizo nazo zimekuwa dhaifu sana na udhaifu huo umesababishwa na vingozi wanaopenda kutawala kwa kutumia njia za mkato – wasiopenda kufuata taratibu za kisheria za kitaasisi. Tumeshuhudia sheria zikivunjwa na viongozi kwa kutoa kauli au matamko ambayo ni kinyume na sheria; watu wananyimwa haki zao za kikatiba na kisheria lakini taasisi husika zinazotakiwa kukemea mambo hayo zimekaa kimya.

**Mheshimiwa Spika,** nikitoa mfano mdogo tu wa uchaguzi wa marudio wa kata 43 za udiwani na ubunge. Ule haukuwa uchaguzi bali ni unyanganyi wa kimabavu kwani kulikuwa na uporaji wa wazi wa karatasi za matokeo ambapo vyombo vya dola vilitumika vibaya kuingilia uchaguzi huo. Lakini Tume ya uchaguzi ambayo ndiyo taasisi yenye dhamana ya kusimamia uchaguzi huo haikutimiza wajibu wa kusimamia chaguzi hizi ipasavyo na hili linatia shaka na kujenga hisia kwamba chombo hiki pengine kinafuata maelekezo kutoka kwa mtu au chombo fulani. Udhaifu kama huo, upo katika taasisi nyingi ikiwemo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa anayeshabikia migogoro ya vyama vya siasa badala ya kuwa msuluhishi.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muda mwafaka sasa kama taifa kuunda taasisi imara zenye uwezo wa kujisimamia na kufanya kazi kwa ufanisi. Mfano; Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) ni lazima iweze kujitathimini katika

utendaji wake ili kuzuia taasisi hiyo kufanya kazi kwa visasi,uwepo wa taasisi inayotathimini utendaji wa Jeshi la Polisi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ofisi ya msajili wa vyama vya siasa nk.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na udhaifu wa taasisi zetu, tumeshuhudia vyombo vya dola kama polisi vikivunja sheria kwa makusudi na watendaji wake wakuu wakijinasibu hadharani kwamba wanafuata maelekezo.Utendaji wa namna hii unajulikana kabisa ni kinyume cha sheria. Lakini hoja ya msingi ni kuwepo na chombo huru inachotathimini utendaji kazi na uwajibishaji wa taasisi hizi ili kupunguza utovu mkubwa wa nidhamu unaofanywa na baadhi ya watendaji wakuu kwa kivuli cha maelekezo kutoka juu.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na taasisi ya kuangalia maadili ya watumishi wa umma, lakini kwa bahati mbaya sana taasisi hii inakosa nguvu ya kufanya kazi kutokana na mashinikizo kwani watendaji wake wakuu ni wateule wa Ikulu. Jambo hili liko wazi kwa kuwa taasisi imeshindwa kuwachukulia hatua wateuliwa wa Ikulu kwenye sakata zima la kuhusu vyeti feki. Pia, tumeshuhudia watendaji wa Serikali ambao ni wateuliwa wa Ikulu wakifanya kazi za uenezi wa Chama cha Mapinduzi. Masuala kama haya yanapelekea wananchi kukosa imani na taasisi hii ya kushughulikia maadili ya viongozi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuboresha utendaji kazi wa taasisi zetu haitawezekana kamwe kuwa na maendeleo endelevu ndani ya nchi yetu. Ni jukumu letu sote kulitazama jambo hili kwa kina na kulifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili kunusuru nchi yetu kuingia katika mipasuko inayotokana na ubaguzi, chuki na visasi na hata kuingia katika majanga yakiwemo machafuko ambayo kimsingi yanaweza kugharimu maisha ya watu wetu, kuporomosha uchumi wetu na kuharibu jina zuri la taifa letu lililolinda misingi ya amani na utulivu tangu uhuru.

## 3. MWENENDO WA HALI YA SIASA, ULINZI NA USALAMA NA ATHARI ZAKE KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

**MheshimiwaSpika,** upo uhusiano wa karibu sana kati ya hali ya siasa, ulinzi na usalama na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Ni ukweli usiobishaniwa kwamba; kama hali ya siasa, ulinzi na usalama katika taifa haipo vizuri; ni dhahiri kwamba kunakuwa na mvurugano wa mambo jambo ambalo ni kikwazo kwa utekelezaji bora wa Mpango wowote wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**hali ya siasa nchini Tanzania kwa sasa si ya kuridhisha. Wapo wanaoona kwamba wao pekee ndio wenye haki ya kufanya siasa na kuharamisha wengine kufanya siasa. Aidha, hali ya usalama ina mashaka. Siku hizi matukio ya utekaji na mauaji yenye kutatanisha yamekuwa ni kawaida katika nchi yetu. Hali kadhalika hali ya ulinzi imedhoofu. Siku hizi kiongozi

kupigwa risasa akiwa maeneo yenye ulinzi, au watu mashuhuri kutekwa katika maeneo yenye ulinzi yamekuwa ni matukio ya kawaida pia.Mazingira yote hayo hayawezi kamwe kuwavutia wawekezaji wakubwa tunaowahitaji katika kuujenga uchumi wetu.Halikadhalika mazingira hayo hayawezi kuwapa motisha wafadhili wetu kutoa fedha za kutekeleza miradi yetu ya maendeleo. Na tayari baadhi ya wafadhili wetu wameanza kukataa kutoa fedha kutokana na mwenendo wa siasa za nchi yetu usioridhisha.

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na watanzania wote wanaopenda kuona haki ikitamalaki katika taifa, tunalaani na tunapinga vitendo viovu vya uonevu, ukandamizaji, utekaji na sasa majaribio ya mauaji yanayofanywa dhidi ya wanachama na viongozi wa vyama vya Upinzani hapa nchini. Ikiwa vitendo hivi vitaachwa viendelee bila kukemewa na kushughulikiwa kwa uzito unaostahili, kuna hatari ya kundi linalohisi kuonewa likakosa uvumilivu na hivyo kuathiri amani ya nchi; na amani ikitetereka, hakuna Mpango wowote wa maendeleo utakaoweza kutekelezwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ni mwaka mmoja na miezi miwili sasa imepita tangu Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu anusurike kifo baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi wakati Mkutano wa Nane wa Bunge ukiwa unaendelea na vikao vyake hapa Dodoma na mpaka sasa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa na Serikali juu ya kukamatwa kwa watu waliohusika na tukio hilo. Ikiwa polisi wameshindwa kufanya uchunguzi na kuwakamata wahalifu hao ndani ya mwaka mmoja

na miezi miwili, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni muujiza wowote unaoweza kutendeka ili watu hao wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria hata kama polisi wataongezewa miaka mingine miwili. Tafsiri ya ukimya huo wa Serikali ni rahisi; kwamba hakuna dhamira ya dhati wala utayari wa kushughulikia jambo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** si nia yangu kuorodhesha matukio mabaya wanayofanyiwa viongozi wa upinzani hapa nchini kwa kuwa ni mengi na pia tumeyasema sana humu bungeni; na wakati mwingine kuamriwa kuyafuta katika hotuba zetu, lakini hili la kutuwinda kwa lengo la kutuuwa, hatuwezi kamwe kulinyamazia. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wananchi wote kupaza sauti zao kupinga uonevu na ukandamizaji wa haki, kupinga matukio ya utekaji, utesaji na umwagaji damu katika nchi. Aidha, tunatoa wito kwa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awaponye wale wote walioathirika na matukio hayo lakini zaidi sana kuliepusha taifa na laana kwa damu ya watu wasio na hatia iliyomwagika katika nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**ili Mpango huu wa Maendeleo tunaoujadili leo uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa, ni lazima tuutekeleze tukiwa na umoja na mshikamano kama taifa. Kamwe haitawezekana kuyafikia hayo maendeleo tunayotaka kwa kubaguana kwa itikadi za kisiasa, au kwa kubezana, kunyanyasana, kuoneana, kuumizana na kuuwana. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa viongozi wote katika ngazi mbalimbali kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu kwa kutenda haki, na kuacha mara moja tabia za ubaguzi,

uonevu, ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya watu wanaowaongoza.

## 4. UWEKEZAJI KATIKA RASILIMALI WATU KWA MAEDELEO ENDELEVUU (INVESTING ON HUMAN CAPITAL FOR SUSTAINABLE DEVELEOPMENT)

**Mheshimiwa Spika,** ni nadharia na uzoefu wa kawaida kwamba; taifa lolote linalotaka kujitegemea na kujinasua kwenye dimbwi la utegemezi na umasikini linajitahidi sana kuwajengea watu wake uwezo wa ki-elimu, ki-ufundi na maarifa ili kuweza kukabiliana changamoto mabalimbali na hivyo kuweza kuyamudu mazingira yao. Kwa sababu hiyo; taifa la namna hiyo, huwekeza sana katika elimu ili kuandaa wataalamu (rasilimali watu) wa kutosha wenye weledi wa kuendesha sekta mbalimbali za uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa sababu hiii, Serikali ya awamu ya kwanza ilikuja na sera ya Elimu ya Msingi kwa Wote - Universal Primary Education na kujikita sana kwenye elimu ya kujitegemea ambayo iliwapatia wengi maarifa ya kujiajiri na kuendesha maisha yao. Hata elimu ya juu iligharamiwa kwa asilimia 100 na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya nchi yetu kuwa bado kwenye dimbwi la umasikini; na licha ya kuwa bado nchi inakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu, Serikali hii ya awamu ya tano imechagua kuwekeza katika vitu badala ya watu. Ni kweli tunahitaji maendeleo ya vitu kama tunavyoona Serikali ikijenga reli ya kisasa, viwanja vya ndege, kununua ndege mpya ujenzi wa mabarabara nk. lakini nachelea kusema kwamba vitu hivyo vinaweza kudumu kwa muda

mfupi mno kama hatutawajengea watu wetu uwezo wa kuvifanya wenyewe na kuviendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani ingefurahi kuona makandarasi wa kujenga reli ya kisasa; na hata mabarabara yetu wakiwa ni watanzania wenzetu. Lakini tathmini fupi inaonyesha kuwa miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchini iko mikononi mwa makandarasi wageni. Watu wetu wanaambulia kazi za kuchimba mitaro, kubeba mizigo na kufanya kazi zile ambazo hazihitaji ujuzi na matokeo yake hata ujira wao ni ule wa mboga tu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ulimwengu wa utandawazi, ufunguo wa mafanikio ya kiuchumi unategemea sana uwezo wa nchi kupata na kutumia ujuzi/maarifa kwa ufanisi na kwa faida katika sekta za kipaumbele na ambazo zinaweza kukua.Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika rasilimali watu, kwa kuwa watu wenye ujuzi ndio msingi mkuu wa kuwepo kwa mfumo wa viwanda unaochochea ukuaji wa uchumi. Uwekezaji katika vitu na katika taasisi ni vikamilisho muhimu vya rasilimali watu; kwani rasilimali (vitu) haitatumiwa vizuri, iwapo itakosa ujuzi wa kiufundi na kiuongozi.

### 4.1. Miradi ya Kimkakati na Maandalizi ya Rasilimali Watu kwa ajili ya Kutekeleza na Kuendesha Miradi Hiyo

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya tano imeeleza katika mpango kuhusu miradi ya kimkakati pamoja na maelezo mengi kuhusu uchumi wa viwanda. Pamoja na miradi hiyo ya kimkakati ambayo imeelezwa na serikali,

haijaelezwa popote kuhusu namna ya kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuendesha na kusimamia miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kutokukubaliana na namna miradi hiyo inavyogharamiwa lakini ni lazima kwa vyovyote huwezi kuendesha miradi kama ya ununuzi wa ndege, reli kwa kiwango cha standard gauge au mradi wa stiglers gorge bila kuandaa wataalam na rasilimali watu ambao wataendesha na kusimamia miradi hiyo ili iweze kuleta tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, haitashangaza kusikia kwamba kwa sasa Shirika la Ndege ndio linapeleka wataalam nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza kuendesha na kusimamia shirika hilo jambo ambalo lingetakiwa kufanyika wakati wa maandalizi ya mradi ili kuwe na mwendelezo wa kuendesha shirika hata baada ya kupata ndege ambazo zinahitaji wataalam.

**Mheshimiwa Spika**, tulishasema na tunaendelea kusema kuwa huwezi kusema uchumi wa viwanda bila kuanza kuhuisha mfumo wetu wa elimu ili uendane na uweze kufikia lengo kuelekea uchumi wa viwanda. Vivyo hivyo huwezi kuwa na miradi mingi ya kimkakati bila kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuiendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri kulieleza Bunge juu ya

mkakati wa kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango hasa kwenye miradi ya kimkakati.

## 5. UDHAIFU WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO KATIKA KUKABILIANA NA MAJANGA NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, mara kadhaa katika nchi yetu tumekumbwa na majanga mbalimbali ya asili ambapo mengine yanatokana na uzembe ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usafiri na mengine yanayotokana na Serikali kushindwa kuchukua hatua za awali na za dharura kabla ya majanga hayo kutokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha sasa tutegemee athari nyingi za kimazingira na majanga ya asili yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi. Mabadiliko ya tabia nchi huathiri sekta karibu zote kama Taifa lisipojiandaa kukabiliana nayo mapema.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haijasahau majanga kama ya tetemeko lilitokea Kanda ya Ziwa Victoria tarehe 10 Septemba, 2016 ambapo Mkoa wa Kagera uliathiriwa zaidi ambapo wananchi wengi walikufa, wengine kukosa makazi, chakula na maji safi na salama. Aidha miundombunu ya elimu pamoja na afya iliathiriwa kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za Serikali vifo vilivyoripotiwa kutokana na tetemeko hilo ni 17, Majeruhi 440, nyumba zilizobomoka 2,063, nyumba zilizopo katika hatari ni 14,081, nyumba zilizopata uharibifu mdogo 9,471 na jumla ya watu ambao walihitaji msaada walikuwa 126,315.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na athari hizo, majibu ya Serikali kwa wananchi kupitia Rais wa nchi ilikuwa "Serikali haijasababisha tetemeko" na kama hilo halitoshi Serikali iliwataka wananchi kujenga nyumba zao wenyewe kwa kuwa Serikali haiwezi kufanya kazi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inachukulia kauli hizo kama kejeli kwa wananchi ambao hutoa ridhaa kwa Serikali iliyopo madarakani kuongoza nchi. Badala Kiongozi Mkuu wan chi kuwa mfariji anageuka na kuwa mtu wa kuongeza machungu kwa wananchi walioathiriwa na janga hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kabla vidonda vya tetemeko havijapona vizuri, hivi karibuni Taifa lilikumbwa na janga lingine kubwa ambapo tarehe 20 Septemba, 2018 Meli ya MV Nyerere ilizamana na kusababisha vifo zaidi ya 200 ambapo ilikuwa ikifanya safari ya Kisiwa cha Bugorora kuelekea Kisiwa cha Ukara.

**Mheshimiwa Spika**, kilichoshangaza katika janga hili ni kuwa shughuli za uokoaji zilisitishwa kwa sababu ya giza huku kukiwa hakuna hatua za dharura kuwaokoa wahanga wa ajali hiyo. Aidha, wahanga wengi waliokolewa na miili mingi kuopolewa kwa kushirikiana na wavuvi wanaofanya shughuli katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, majanga haya mawili nimeyaeleza kwa sababu ni ishara kwamba Serikali hii ya CCM haina mkakati wala nia ya kuhakikisha kuwa inakuwa na bajeti, vifaa na kutumia teknolojia kukabiliana na majanga nchini.

**Mheshimiwa Spika**, nayasema haya kwa sababu, licha ya mabadiliko ya tabia nchi kuathiri kila sekta kama nilivyoeleza awali; bado hakuna kipaumbele chochote

kinachopewa eneo hili. Ukirejea Randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu (fungu 37) kwa mwaka wa fedha 2017/18, kifungu 2001 mradi namba 6575 "***Kujenga Uwezo wa Kujiandaa na Kukabili Maafa"*** hakuna fedha yoyote ya ndani iliyokuwa imetengwa kwa ajili shughuli hiyo. Fedha za nje zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo zilikuwa ni shilingi 440,000,000/; lakini hadi mwezi kufikia mwezi Februari 2018 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, katika kifungu hicho cha 2001 mradi namba 5306 "***Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadhari"*** haukuwa umetengewa fedha yoyote ya ndani. Fedha ya nje ilikuwa ni shilingi 1,021,618,000/- na hadi mwezi februari 2018 zilikuwa zimetolewa shilingi 283,986,200 sawa na asilimia 28.7 pekee.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka huu 2018/2019 kifungu hicho 2001 chenye miradi hiyo hiyo hakikutengewa fedha yoyote ya ndani. Fedha za nje zilizotengwa ni shilingi 176,530,200/- kwa maradi namba 6575 na shilingi 286,923,269/- kwa mradi namba 5306. Hata hivyo fedha hizo zimepungua ukilinganisha na mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** wakati nchi yetu imeridhia mikataba ya kimataifa kuhusu namna ya kukabiliana na athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi; lakini kinachofanyika ndani hasa suala la kutenga na kutekeleza bajeti kuhusu masuala hayo ni kinyume na jinsi ilivyokuwa imekubaliwa.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba Tanzania imekuwa inachukua hatua mbalimbali katika kuelezea mabadiliko

ya tabianchi kwa muktadha wa nchi yetu na hivyo kutayarisha nyaraka muhimu za mkakati kama vile "The National Climate Change Strategy (2012) and the Zanzibar Climate Change Strategy (2014)" ambazo zinaeleza kwa kina hatua za kuchuka katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabinanchi. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini kila mara inashindwa kutenga na kutoa fedha za ndani ikiwa kulikuwa na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabia Nchi?.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utelelezaji wa Mpango Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka 2016/2017-2018/2019 cha Oktoba, 2018 ambacho amewasilisha Waziri katika Bunge lako tukufu ukurasa wa 14 miradi namba 48 na 49 yaani kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa na kuimarisha taarifa za mabadiliko ya tabianchi na uboreshaji wa mifumo ya tahadhari za awali serikali haikutenga hata senti kwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa Serikali imewaacha wahisani kushughulikia dhamana ya watu wetu kwa sababu katika taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo wahisani walitoa fedha walizoahidi kwa zaidi ya 95% huku serikali ikitenga na kutoa sifuri katika miradi hiyo hiyo. Katika hali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani haikushangaa kuona Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akisitisha shughuli za uokoaji kwa sababu ya kuingia kwa giza.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame wa muda mrefu, mvua kubwa

zinazosababisha mafuriko na ambapo athari hizo huathiri shughuli za kiuchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla, kwa sababu hiyo tunaitaka Serikali kuanzisha mfuko wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na sio kutenga sifuri katika bajeti kwa miaka miwili mfululizo huku nchi ikiendelea kukumbwa na majanga mbalimbali ambayo athari ni kubwa na kuangamiza maisha ya watu.**Aidha,ni wakati muafaka sasa Serikali ikaishirikisha Sekta Binafsi katika kukabiliana na majanga.** Sekta Binafsi ingekuwa imepewa nafasi katika masuala ya kukabiliana na majanga na uokozi, yamkini vifo vilivyotokea wakati wa kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere vingeweza kuepukwa.

## 6. UHUSIANO WA KIMATAIFA NA ATHARI ZAKE KATIKA MIPANGO YA SERIKALI

### 6.1. Ukakasi Kuhusu Mradi wa Reli ya Standard Gauge railway na Uhusiano wa Kimataifa

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani katika uchambuzi wake imerejea kitabu cha Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya mwaka wa fedha 2018/19 katika ukurasa wa 18, Serikali imeeleza kuwa Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini China tarehe 17 hadi 20 Desemba, 2017 ambapo serikali inaeleza pia kuwa katika ziara hiyo Waziri aliwasilisha kwa serikali ya China miradi ya kimkakati ambayo Serikali inategemea kuitekeleza ikiwemo mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), kusafirisha umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze na Chalinze hadi Dodoma, mradi wa kufua umeme wa Stiglers Gorge,

ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda na ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa Ndege wa Mwanza.

**Mheshimiwa Spika**, katika maelezo ya serikali hakuna sehemu ambayo wameonyesha wala kueleza idadi ya miradi ambayo serikali imeshaingia makubaliano ya awali na serikali ya China kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, sote tunatambua kuwa taarifa zilizokuwa kwa umma ilikuwa makubaliano ya awali kati serikali ya Tanzania yalishafikiwa kuhusu China kushiriki katika ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR). Ni jambo gani ambalo lilipelekea China kujitoa katika mradi huo?

**Mheshimiwa Spika**, sote tunambua kuwa kwa sasa SGR inajengwa na Kampuni kutoka Uturuki, lakini kama tulivyoeleza kuwa wakati wa serikali ya awamu ya nne taarifa zilitolewa kuwa China ndiyo itakayojenga SGR kwa mkopo kutoka Bank ya Exim ya China. Kama Waziri na serikali kwa ujumla walilitambua hili, ni sababu gani ilimfanya Waziri wa Mambo ya Nje kwenda tena China kufanya majadiliano kuhusu mradi huo ambao wamebadili mkandarasi? Kuna tofauti gani kwa maslahi ya Taifa ambayo tumeipata kuwaacha Wachina na kwenda kwa Waturuki?

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo ya Serikali bado kuna mkanganyiko kuhusu namna ugharamiaji wa mradi wa SGR kwa kuwa mara kadhaa Rais Magufuli amenukuliwa akisema kuwa SGR inagharamiwa na fedha za ndani kwa asilimia 100, wakati huo huo Waziri wake wa Mambo ya Nje anazunguka kwenye mataifa ya nje kutafuta ufadhili. Ukweli ni upi?

**Mheshimiwa Spika**, aidha hivi karibuni Waziri wa Fedha na Mipango alinukuliwa na vyombo vya habari akiomba Benki ya Barclays kuona namna ya kutoa mkopo kwa serikali kugharamia ujenzi wa SGR. Je serikali inafaidika na nini kwa kutoa kauli tofauti tofauti kuhusu ugharamiaji wa mradi huu?

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Jarida la The Economist Intelligence inaonesha kuwa kuna ugumu kupata mikopo ya ujenzi wa miradi nchini Tanzania na pia hakuna uwazi kuhusu gharama na lini miradi hiyo itakamilika jambo ambalo linatoa taswira hasi kwa wawekezaji na taasisi za fedha za kimataifa. Aidha, kitendo cha kukosekana kwa uwazi kama ni fedha za nje au ni za ndani zinatumika kujenga SGR kunatoa ishara ya mazingira ya ufisadi.

### 6.2. Tathmini ya Mafanikio ya Kiuchumi ya SGR

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kwamba ujenzi wa Reli kwa kiwango cha Standard gauge (SGR) utatoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Katika hali ya kushangaza tarehe 20 Septemba, 2018 jarida la Expogroup liliripoti kuwa Tanzania imepata mkopo wa dola bilioni 1.4 ambazo ni zaidi ya trilioni 3 kutoka Benki ya Standard Chartered kwa ajili ya kugharamia kipande cha Morogoro hadi Makutupora Dodoma[3].

**Mheshimiwa Spika**, habari hiyo ni tofauti na maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa na Rais Magufuli kuwa

[3]https://www.expogr.com/tanzania/buildexpo/detail_news.php?newsid=5472&pageid=2

tunajenga Reli ya kati kwa fedha zetu wenyewe. Kwa sababu jarida hilo limemnukuu Waziri wa Fedha, ni vema akalieleza Bunge lako tukufu kuhusu utaratibu wa ugharamiaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuhusu ujenzi wa kipande cha reli kwa kiwango cha SGR kutoka Isaka kwend Rusumo lakini haijaeleza ujenzi huo kutoka Makutupora hadi Tabora na Tabora hadi Isaka.

**Mheshimiwa Spika**, ni vema Serikali ikalieleza Bunge sababu za kiuchumi za kwa nini wajenge reli hiyo mpaka mwanza na rusumo kabla kwanza ya kujenga reli hiyo kutoka Tabora hadi Kigoma kwa ajili ya kufungua fursa za nchini ya DRC.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapenda kuona reli hiyo ikifungamanishwa na uchumi katika maeneo ya kimkakati na sio kuelezwa muda wa kusafiri kwa treni ya reli ya kisasa kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam. Hii ni kwa sababu Kambi Rasmi inaamini kuwa mradi huo hautakuwa na tija kwa kulenga tu kupunguza muda wa abiria kusafiri bali kuufungamanisha na sekta nyingine za uchumi kwa ajili ya kuleta tija.

### 6.3. Ushiriki Hafifu wa Nchi yetu katika Mikutano ya Kimataifa ya Kimkakati Unavyoweza Kuathiri Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni mwaka 2017/2018 tulieleza kwa kirefu kuhusu umuhimu wa Rais kufanya ziara za kimkakati nje ya nchi ikiwemo kushiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kongamano la Kiuchumi Duniani na mikutano mingine ambayo kiongozi wa nchi anabeba taswira ya Taifa letu kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, msimamo wa Rais kwa sasa ni kutosafiri kwenda nje ya nchi, jambo ambalo kama Kambi tunaona nchi inashindwa kupata fursa ambazo tungezipata kwa kushiriki mikutano na makongamano ya kimataifa ya kimkakati.

**Mheshimiwa Spika**, imefikia hatua Makamu wa Rais anazidiwa kuiwakilisha nchi katika mikutano ya kimataifa wakati Rais wa nchi yupo. Mfano mdogo ni kongamano la hivi karibu la nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola ambapo viongozi wengine wa Afrika Mashariki walifanya vikao vingi vya kimkakati na wadau wengine wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ukitazama picha ambazo zilisambaa mtandaoni kuhusu vikao vya kimkakati alivyofanya Rais wa Jamhuri ya Kenya Uhuru Kenyatta; na alivyofanya Makamu wetu wa Rais na wadau wa maendeleo wakati walipohudhuria Kongamano la nchi wananachama wa Jumuiya ya Madola utaona tofauti kubwa sana. Vikao vya Rais Kenyatta vilikuwa vingi na alikutana na wadau mbalimbali wa maendeleo tofauti na vikao alivyofanya

Makamu wetu wa Rais vilikuwa vichache na pia wadau wachache. Hii inatoa taswira jinsi ambayo kama nchi hatupo makini kwenye masuala ya kidiplomasia.

**Mheshimiwa Spika**, gharama za safari za nje zisitumiwe kama kisingizio cha Rais kutohudhuria mikutano ya kimataifa bali utazamwe umuhimu wa ziara hizo kwa nchi kwa ajili ya kujenga diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni umezuka utamaduni wa kuwahusisha viongozi wastaafu kwenye mikutano ya kimataifa. Mara kadhaa ameonekana Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete katika mikutano kadhaa ya kimataifa bila kuelezwa wazi kama analiwakilisha Taifa au ameenda kwa mwaliko binafsi katika mikutano hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwenye kitabu chake cha randama uk. 25 serikali inaeleza yafuatayo;

"***Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Abdulrahman Kinana kwa ajili ya kumwakilisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye sherehe za uapisho wa Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Rwanda tarehe 18 Agosti, 2017***"

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo ya Wizara ni ukweli kuwa kwa sasa viongozi wastaafu wanaiwakilisha serikali kwenye masuala ya kimataifa. Hoja ya msingi hapa ni je wastaafu ambao hawana mamlaka ya kiserikali tena, kwa sasa wanayo mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya serikali?

**Mheshimiwa Spika**, serikali imekiri na kuthibitisha kuwa imefikia hatua hata Katibu Mkuu wa CCM anagharamiwa na fedha za walipakodi kuiwakilisha serikali kwenye masuala ya uhusiano wa kimataifa. Tabia kama hii ni ishara kuwa serikali inayo nia ya kuigeuza nchi hii kuwa ya Chama kimoja kwa sababu serikali imeanza kukifanya chama kushiriki kwenye hafla za kimataifa kwa gharama za fedha za walipa kodi ambao sio wote wanakiunga mkono Chama cha Mapinduzi.

### 6.4. Ukiukwaji wa Haki za Binadamu na Taswira ya Taifa letu Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili mwaka huu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilizindua taarifa yake ya mwaka 2017 ambapo jambo kubwa ambalo lilionekana kwa mwaka huo ni Watu Wasiojulikana walivyo Tishio la Haki za Binadamu nchini. Pamoja na taarifa hiyo, taarifa ya Mambo ya Ndani ya Marekani kuhusu Tanzania imeeleza na kuonesha matukio kadhaa ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha tarehe 10 Mei, 2018 asasi za kiraia 65 duniani zilimwandikia barua Rais Magufuli kuitaka serikali yake kuangalia namna ya kushughulikia tishio la mazingira mabaya kwa waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na vyama vya upinzani.

**Mheshimiwa Spika**, Asasi hizo za kiraia zimeeleza wasiwasi wao kuhusu hali ya watu kupotea, matukio ya watu wasiojulikana kama vile kupigwa risasi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, kutekwa kwa Azory Gwanda na hivi karibuni kutekwa kwa Mfanyabiashara mkubwa nchini Mohamed Dewji, kuzuiwa kwa shughuli za kisiasa, kuminywa kwa

uhuru wa kutoa maoni na kujumuika, kutumia sheria kandamizi kudhibiti vyombo vya habari na uhuru wa kutoa maoni.

**Mheshimiwa Spika**, Asasi hizo za kiraia zimeionya serikali kuwa ule msemo na sifa ya Tanzania kama kisiwa cha amani itapotea kama serikali isipochukua hatua za dharura kudhibiti hali mbaya ya kumomonyoka kwa misingi ya haki za binadamu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Wameshauri kuwa vifungu vyote vya Sheria ya Makosa ya Mtandao na Kanuni mpya za matumizi ya mitandao zilizotangazwa na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo zifutwe, kuvifutia adhabu vyombo vyote vya habari ambavyo vimeadhibiwa, uchunguzi huru ufanyike dhidi ya matukio ya utekaji, utesaji, kupotea kwa watu na wengine kushambuliwa kwa risasi pamoja na kuhakikisha kuwa uhuru wa watu wa kujumuika kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa unazingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, imefikia hatua hata vyombo vya dola ambavyo kimsingi vilitakiwa kulinda wananchi na mali zao sasa vimekuwa sehemu ya mauaji na utesaji wa wananchi. Hili ni tatizo na janga kwa taifa kwa sababu Tanzania sio kisiwa ni sehemu ya Jumuiya za Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na kigugumizi kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya utesaji na kutwezwa (**International Convention Against Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment**) jambo ambalo linatoa taswira mbaya kwamba haina mpango wa kulinda haki za binadamu hapa nchini. Kutokana na mlolongo wa matukio haya ya

utesaji, utekaji, kupigwa risasi kwa wananchi na mauaji katika vituo vya Polisi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka sasa Serikali kuuleta mkataba huo bungeni ili uridhiwe na Bunge ili matukio hayo ya ukiukwaji wa haki za binadamu yaweze kukomeshwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa matukio ambayo yanatokea nchini kwa sasa yanayofanywa na watu wasiojulikana ni wazi kuwa taswira ya Tanzania katika sura ya kimataifa imechafuka na ni lazima serikali ichukue hatua. Kama serikali inaziba masikio kwenye mambo kama haya taifa letu litatengwa na Jumuiya ya Kimataifa. Matokeo ya kutengwa au kunyooshewa kidole na Jumuiya ya Kimataifa kuna athari kubwa sana katika uchumi kwa kuwa bado Serikali inategemea misaada mingi ya kibajeti kutoka katika Jumuiya ya Kimataifa lakini pia pia watalii na wawekezaji ambao ni sehemu muhimu ya ujenzi wa uchumi wetu wataacha kuja kutokana na hofu ya usalama wao na hivyo kuathiri ukuaji wa uchimi wetu.

### 6.5. Serikali Kushindwa Kuitumia Diaspora Kiuchumi

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imeshazungumza vya kutosha kuhusu umuhimu na namna serikali inavyoweza kuwatumia Watanzania wanaoishi na kufanya kazi katika mataifa mbalimbali duniani (**Diaspora**) kwa ajili kushiriki katika kujenga uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, tulishawahi pia kushauri kuwa ili kuwe na uhusiano wa moja kwa moja kati ya nchi na Diaspora ni vema serikali ikaona haja ya kuwa na utaratibu wa uraia wa nchi mbili/ uraia pacha kama baadhi ya mataifa mengine yalivyofanya na kuendelea kunufaika

na watu hawa ambao kimsingi ni Watanzania wenzetu. Zipo hoja kinzani zilizowahi kujengwa kuhusu pendekezo hili na mojawapo ni uwezekano wa kukosekana kwa uzalendo ikiwa Mtanzania atakuwa raia wa nyingine bila kuathiri uraia wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Tumeshawahi pia kueleza namna nchi za Kenya, Ghana, Nigeria, Misri, Ethiopia na Afrika ya Kusini zinavyonufaika na kuwatumia vizuri Diaspora ambapo mapato yanayotokana na Diaspora (Remittance) yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2010 pekee taarifa ya Benki ya Dunia inaonyesha kuwa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 40 ulikuwa mchango wa Diaspora kwa bara zima la Afrika. Taarifa hiyo inaonyesha pia kuwa akiba ya Diaspora kwa mwaka ilikadiriwa kuwa zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 53[4].

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania imetajwa kuwa moja ya nchi 12 zenye Diaspora wengi katika nchi ya Canada. Je serikali imeweka mkakati gani kuwatumia watu hawa kunufaika na masuala ya biashara, uwekezaji, teknolojia na fursa za mikopo ya masharti nafuu?

**Mheshimiwa Spika**, ni vema serikali ikafahamu kuwa kwa kushirikiana na Diaspora tunaweza kunufaika na utaratibu wa PPP kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo kuliko sasa ambapo fedha za ndani nyingi zinatumika kwenye miradi mingi ambayo faida yake haitapatikana hivi karibuni na mikopo yenye masharti magumu.

---

[4]http://siteresources.worldbank.org/EXTDECPROSPECTS/Resources/476882-1157133580628/DfD_FullReport.pdf

**Mheshimiwa Spika**, katika hali ya kushangaza umeibuka utaratibu wa serikali ya awamu ya tano ya kuwakamata Watanzania ambao wanafanya kazi na kuishi nje ya nchi wakiwa kwenye Viwanja vya ndege wakiwa na fedha zao na kuwapa tuhuma za uhujumu uchumi au utakatishaji fedha. Utaratibu huu unaanza kuwarudisha nyuma Diaspora kuingiza fedha nchini kwa ajili ya shughuli zao binafsi na shughuli za kibiashara. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani utaratibu huu ambao unazuia nchi yetu kunufaika na Diaspora. Serikali isijifiche kwenye makosa ya uhujumu uchumi au utakatishaji fedha kwa sababu makosa hayo yalikuwepo na utaratibu wa kuingiza fedha za kigeni unajulikana.

## 7. NAFASI YA SEKTA BINAFSI KATIKA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani ya Januari 2018 kuhusu mapitio ya saba ya Mwongozo wa Sera ya Tanzania[5] imeeleza pamoja na mambo mengine kuwa pamoja na pato la taifa kuonekana kukua mazingira ya biashara nchini sio rafiki kwa uwekezajina maendeleo ya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo ya sasa, inaonekana dhahiri kuwa shughuli za kiuchumi ni dhaifu na hivyo kupelekea kushindwa kuzalisha ajira na kupunguza umasikini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa pamoja na taarifa ya biashara nyingi kufungwa ambayo tulieleza kwa kirefu katika hotuba yetu ya mpango kwa mwaka uliopita, Waziri wa Fedha alijibu kwa idadi ya biashara mpya zilizofunguliwa

[5] IMF Country Report No. 18/11 The Seventh Review Under The Policy Support Instrument.

na kueleza kwa propaganda kuwa biashara zilizofungwa zilikuwa zinahusishwa na ukwepaji kodi.

**Mheshimiwa Spika**, kufungwa kwa biashara nchini sio jambo la kushangilia kwa sababu ni dhahiri kuwa wafanyabiashara hao walikuwa wanalipa kodi, na hivyo kuongezeka kwa makusanyo. IMF wanaeleza kuwa makusanyo ya kodi yameshuka tofauti najinsi ilivyokuwa inategemewa na hivyo kupelekea utekelezaji wa bajeti ya serikali kuwa dhaifu.

**Mheshimiwa Spika**, aidha bado mikopo isiyolipika katika mabenki ni tatizo kubwa pamoja na takwimu za Serikali kuonyesha kuwa Benki Kuu imetoa maelekezo kwa Mabenki kupunguza mikopo chechefu, jambo hilo ambalo linaathiri pia mazingira ya ufanyaji biashara kwa sababu kutokana na madhaifu yaliyopo katika mfumo wa sasa kodi na maelekezo ya kiutawala yasioangalia maslahi ya wafanyabiashara hupelekea wafanyabiashara kushindwa kulipa mikopo kwenye mabenki ya ndani[6].

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa mara nyingine tena inakiri katika taarifa zake kuwa ukuaji wa mzunguko wa fedha nchini bado ni chini ya 12% ikilinganishwa na ukuaji wa 16.4% kwa mwaka ulioishia Julai 2015[7]. Tafsiri ya hali hii ni kuwa tusitarajie wananchi kuwa na ahueni kama mzunguko wa fedha bado uko chini kiasi hiki na pia tusitarajie sekta binafsi kuendelea kukua katika awamu hii ya tano.

---

[6] Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti, Oktoba 2018 ukurasa wa 13
[7] Ibid, ukurasa wa 12

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Rais inajinasibu kuwa mfumuko wa bei umepungua nchini, huku wakishindwa kuelewa kuwa kama mzunguko wa fedha ni mdogo kama ambavyo wanakiri katika vitabu vya mpango, hali ya sekta binafsi nchini iko taabani, mikopo katika mabenki hailipiki, watumishi wa serikali hawaongezewi mishahara wala posho, kupunguzwa kwa wafanyakazi katika mashirika ya umma na binafsi, hakuna kipya kwenye hili kwa sababu ni ishara na ni wazi kuwa uwezo wa wananchi kununua umepungua na hivyo ni lazima mfumuko wa bei utakuwa chini.

**Mheshimiwa Spika**, sio chini ya miezi sita iliyopita Rais alipokea kinachoitwa gawio kutoka katika Shirika la Simu la TTCL huku Rais akipongeza 'management' ya shirika na kuwataka waongeze mishahara kwa watumishi. Kabla Watanzania hawajasahau, Mkurugenzi Mtendaji amenukuliwa na Vyombo vya Habari akieleza kuwa Shirika linatarajia kupunguza Wafanyakazi 555. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuihoji Serikali juu ya uhalisia wa gawio hilo na kile ambacho kimetangazwa hivi karibuni cha kupunguza wafanyakazi. Ni vema pia Serikali ikafahamu athari za kucheza na mahesabu ya uchumi kisiasa na kipropaganda kwa sababu mara zote hesabu hazidanganyi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya IMF pia inaeleza kuwa hadi kufikia mwezi Septemba mwaka 2017 mikopo isiyolipika katika mabenki ya biashara iliongezeka kutoka asilimia 9.1 hadi 12.5.Hali hii ilipelekea mabenki nchini kupata hasara kubwa jambo ambalo halijawahi kuwepo toka mwaka 2007.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hatua za Benki Kuu kupunguza kima cha chini cha fedha zinazohitajika kuhifadhiwa na Benki za Biashara nchini ikiwa ni pamoja na kushusha kiwango cha riba bado sekta hiyo ilifanya vibaya na hivyo kuathiri mazingira ya biashara katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, mauzo ya bidhaa kwenda nje ya nchi (export) yalionekana kushuka na pia makusanyo ya ushuru wa bidhaa nayo yalishuka kutokana na wananchi kupunguza matumizi ya bidhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuangalia kwa umakini hali ya uchumi wa nchi kuliko kuendelea kutoa kauli za kuwashawishi wananchi kuwa hali ni nzuri wakati katika takwimu hali inaonekana tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, serikali haiwezi kukusanya kodi ya kutosha kama mazingira biashara na sera za kodi ziko hovyo. Aidha serikali haitapiga hatua kama maamuzi ya namna ya kuboresha biashara yanafanywa na serikali kuu bila hata kuzingatia uhalisia wa mazingira ya biashara. Ikumbukwe kuwa serikali imejinasibu kupunguza matumizi ya kawaida kwa ajili ya kubana matumizi, jambo hili ni jema hasa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Kupunguza matumizi kwa sekta muhimu ambazo wafanya biashara walikuwa wanaingia mikataba ya kibiashara pamoja na zabuni za serikali usitegemee kukua kwa biashara nchini kwa sababu serikali ndiyo inayohitaji huduma na kupata huduma na bidhaa ni lazima ishirikishe sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, yapo pia malalamiko ya wazabuni ambao walikuwa na madeni na serikali kwa sababu ya

huduma au bidhaa ambazo walihudumia katika taasisi mbalimbali za serikali ambao hawajalipwa na serikali inasema bado inahakiki madeni hayo kama ni halisi. Wahanga wa uhakiki huu ni wafanya biashara ambapo pamoja na kushindwa kuendelea kufanya biashara kwa sababu ya madeni, hata madeni hayo yakilipwa bado hayalipwi kulingana na bei ya soko au kuangalia na thamani ya shilingi yetu ambayo bado inasuasua.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge kupitia Kamati zake za kisekta zinazohusika na masuala ya uwekezaji na biashara nchini kuangalia hali hii ambayo si njema katika mustakabali wa Taifa letu na kuchukua hatua za dharura kuisimamia serikali ili kuepuka anguko la uchumi ambalo linakuja mbeleni.

**Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa maendeleo wa taifa 2018/2019 inazungumzia mazingira mazuri ya uwekezaji nchini. Ifahamike kuwa katika taarifa iliyotolewa na Bank ya Dunia ya 'Doing Business 2019: Economy Profile Tanzania' inaonyesha bado Tanzania ni moja ya nchi yenye mazingira magumu katika uwekezaji wa kibiashara. Ni nchi ya 163 duniani katika unafuu wa uanzishaji wa biashara (starting a business).Pamoja na hayo Tanzania ni nchi ya 150 katika utika ukiritimba wa vibali vya ujenzi,ni nchi ya 146 duniani katika uwezeshaji wa usajili wa biashara, ni nchi ya 167 katika malipo ya kodi ikiwa na maana kuwa ina kodi nyingi katika

mazingira ya kuanzisha biashara, na ni nchi ya 131 katika kuwalinda wawekezaji (Protecting minority Investors).[8]

**Mheshimiwa Spika**, Hii ikiwa na maana kwamba bado serikali yetu haijaweza kuthamini mchango wa sekta binafsi nchini na kuipa kipaumbele kinachostahili. Nchi kama Kenya ambayo ni nchi majirani wamejitahidi katika kuhakikisha uanzishaji wa biashara na kuwalinda wawekezaji ni moja ya kipaumbele muhimu ambacho kinachochea kukua kwa sekta binafsi nchini humo. Mpaka sasa Kenya ni nchi ya 61 duniani katika kuhamasisha mazingira mazuri ya uwekezaji huku nchi kama Botswana ikishika nafasi ya 86. Hivyo ni wakati muhimu sasa kwa wataalamu wetu kujifunza kutoka kwa wenzetu ili kujua ni mbinu gani za kimsingi ambazo wametumia ili kuweza kuwavutia wawekezaji, kupanua sekta binafsi na kuishirikisha sekta binafsi katika maedeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani katika sera yake ya kushirikisha sekta binafsi katika maendeleo ya nchi inalenga kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji, uanzishaji wa biashara nchini, mifumo mizuri ya

---

[8] http://www.doingbusiness.org/content/dam/doingBusiness/country/t/tanzania/TZA.pdf

kikodi na kuwa na sheria na kodi zinazotabirika ili serikali na sekta binafsi ziweze kushirikiana kwa ufanisi katika kukuza uchumi wa nchi

### 7.1. Ushirikishwaji Hafifu wa Sekta Binafsi katika Uwekezaji kwenye Sekta ya Miundombinu

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inafanya uwekezaji kwenye reli ya *standard gauge* (SGR), Mradi wa umeme wa Stiegler'sGorge, bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Tanga na mradi wa Bandari ya Bagamoyo ambao kwa sasa hauzungumziwi sana lakini hakuna mkakati wa wazi wa namna miradi hiyo inagharamiwa.

**Mheshimiwa Spika**, mara kadhaa Rais John Magufuli anasikika akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za ndani za walipa kodi, na wakati mwingine Waziri wa Fedha ananukuliwa akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za mikopo mbalimbali. Hata hivyo kutokuwa wazi kuhusu gharama za miradi mikubwa na muda wa kuimaliza kunazua sintofahamu kuhusu uwezekano wa kumaliza miradi hiyo mikubwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kuwa kama serikali haitashirikisha sekta binafsi kupitia ubia (PPP) wachambuzi wa uchumi wameshauri kuwa deni la taifa litaendelea kukua na kuwa mzigo kwa walipa kodi. Aidha ikumbukwe kuwa serikali imekua ikikopa sana ndani na hivyo kutengeneza ushindani na wawekezaji wa ndani ambao pia wanatumia mikopo kuendeleza biashara zao.

**Mheshimiwa Spika**, Ushirikishwaji wa sekta binafsi sio utachochea tu mazingira ya biashara na mzunguko wa fedha nchini bali pia itaipunguzia serikali mzigo wa kuwekeza kwenye kila mradi mkubwa jambo ambalo linasababisha ugumu katika kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje na kuepuka serikali kukopa sana ndani kugharamia miradi hiyo.

## 8. UTEKELEZAJI DUNI WA BAJETI YA SERIKALI UNAVYOKWAMISHA MIPANGO YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,**tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani, kumekuwa na utamaduni mbovu wa kupanga bajeti na kushindwa kuitekeleza jambo ambalo limekwamisha miradi mingi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**Kushindwa kwa Serikali kutekeleza kikamilifu bajeti yake kunatokana na sababu mbalimbali. Mosi, ni kuweka makisio makubwa ya makusanyo ya fedha; na kushindwa kukusanya kiasi hicho. Kile kiasi kilichoshindikana kukusanya kinakuwa ni makusanyo hewa; na ile miradi ambayo ilitakiwa kutekelezwa na kiasi hicho kilichoshindikana kukusanywa huwa haitekelezwi kabisa. Kwa mfano:-

- Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 29.54 lakini iliweza kukusanya mapato kutoka vyanzo vyote yaliyofikia shilingi trilioni 20.7 sawa na asilimia 70.1 ya lengo. Hii ina maana kwamba, asilimia takriban 30 iliyobaki (sawa na shilingi trilioni 8.83) ilikuwa ni makusanyo

hewa, na miradi iliyotakiwa kutekelezwa na kiasi hicho haikutekelezwa.

- Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 31.71 lakini iliweza kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 21.89 sawa na asilimia 69 ya lengo. Hii ina maana kwamba asilimia 31 iliyobaki (sawa na shilingi trilioni 9.82) ilikuwa ni hewa na kwa maana hiyo haikutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sababu ya pili, ni kutotekeleza kikamilifu bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika sekta mbalimbali. Nitatoa mifano katika wizara tatu zinazogusa maisha ya watu wengi moja kwa moja kwa miaka miwili (2016/17 na 2017/18):-

i. **Wizara ya Kilimo:-**

- Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Kilimo iliidhinishwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 100.527 lakini hadi Machi, 2017 zilitolewa shilingi bilioni 2.252 sawa na asilimia 2.22 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 98 ya bajeti hiyo haikutekelezwa.

- Katika mwaka wa fedha 2017/18; wizara hii iliidhinishiwa na Bunge fedha za maendeleo jumla ya shilingi bilioni 150.253

(**150,253,000,000/-)** lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018; ni shilingi bilioni 16.5 tu (**16,520,540,444/-)** zilikuwa zimetolewa ikiwa ni sawa na **asilimia 11 tu** ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa. Hii ina maana kwamba asilimia 89 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo haikutekelezwa.

ii. **Wizara ya Mifugo na Uvuvi:**

- Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4 lakini zilizotolewa ni shilingi milioni 130 tu sawa na asilimia 3.25 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba,takribani asilimia 97 ya bajeti hiyo, haikutekelezwa.

- kwa mwaka wa fedha 2017/18 Wizara hii iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 4 **(4,000,000,000/=)** kama fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi; lakini hadi kufikia mwezi machi, 2018 hakuna hata shilingi moja ambayo ilikuwa imepokelewa kutoka hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo

katika sekta hizo. Hii ina maana pia kwamba asilimia 100 ya bajeti ya maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi haikutekelezwa kwa kipindi hicho.

### iii. Wizara ya Maji

- Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 913.836 lakini zilizotolewa zilikuwa ni bilioni shilingi 230.997 sawa na asilimia 25 ya fedha iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba, asilimia 75 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji kwa mwaka huo haikutekelezwa.
- Kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 623.606 lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018, fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 135.191 sawa na asilimia 22 ya fedha zilizoidhinishwa. Hii ina maana pia kwamba asilimia 78 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji haikutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sababu ya tatu inayoifanya Bajeti ya Serikali ishindwe kutekelezwa ipasavyo ni Utovu wa Nidhamu ya Matumizi ya Fedha kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Sheria ya Fedha.Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kifungu cha 41(1) ni kwamba; Ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutekeleza majukumu ya Serikali *"Serikali itatakiwa kuwasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa"*. Aidha, utaratibu huu unatiliwa nguvu na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001( Public Finacne Act, 2001)ambapo kifungu cha 18 (3) na (4) kinaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza (mini-budget) kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huo wa kisheria umekuwa ukivunjwa na Serikali kwa kufanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge jambo ambalo linaua dhana ya madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali; lakini pia kunatoa mwanya wa wizi na ubadhirifu wa fedha za umma. Ikiwa matumizi yanafanyika nje ya bajeti; bajeti ya namna hiyo haina uhalali kuwa haina baraka za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** upotevu wa fedha wa shilingi trilioni 1.5 uliobainika na CAG yamkini unatokana na matumizi ya fedha kiholela yanayofanywa na Serikali bila kuidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** ipo mifano mingi ya mtumizi ya Serikali yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa na Bunge. Mifano hiyo ni pamoja na:-

- Ujenzi wa Ukuta kwenye machimbo ya Tanzanite – Mirerani
- Ujenzi wa Hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege – Chato
- Kuhamishia Makao Makuu Dodoma bila bajeti ya kufanya hivyo zoezi hilo kutumia fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, utovu wa nidhamu ya matumizi yay a fedha zilizoidhinishwa na Bunge umekwenda mbali zaidi kwa kuzipatia baadhi ya wizara nyongeza ya fedha katika bajeti zake tofauti na zile zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge kuhusu matumizi ya serikali kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 na mwelekeo hadi Juni 2018 inaonyesha kwamba baadhi ya wizara zilipatiwa fedha zaidi ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

i. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambapo bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, ilikuwa ni shilingi 4,616,070,000; lakini kiasi kilicholipwa hadi kufikia Machi 2018 ni shilingi 8,880,870,019 sawa na **(257%)**

ii. Tume ya Uchaguzi:- bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 2,470,031,000. Kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 kilikuwa ni shilingi 6,031,856,200 sawa na **(326%)**

iii. Ofisi ya Rais (TAMISEMI), bajeti iliyidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 8,212,296,000. Kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018,kilikuwa shilingi 17,122,775.005 sawa na **(278%)**

iv. Wizara ya Mambo ya ndani: - Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 4,405,897,000; lakini kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 kilikuwa ni shilingi 11,318,896,430 sawa na **(343%)**

v. Ofisi ya Makamu wa Rais:-Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 2,879,167,000; lakini kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 ni shilingi 5,811,478,145 sawa na **(269%)**

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi yote haya ambayo hayakujumuishwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa na Bunge yanaifanya Bajeti ya Serikali kutotekelezeka ipasavyo kwa kuwa fedha hizo za nyongeza kwa baadhi wizara nilizotaja yamkini zimetolewa kwenye miradi mingine na kwa maana hiyo miradi hiyo haikutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** nimetoa mifano hiyo michache lakini ukifanya uchambuzi wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kutekeleza miradi mbalimbali utakuta

kwamba zaidi ya asilimia 60 ya fedha hizo hazikutolewa; na kwa maana hiyo miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na fedha hizo haikutekelezwa. Kwa mantiki hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili; ni kwa nini inawahadaa wananchi kwa kutoa makisio makubwa ya bajeti ambayo kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikishindwa kuyafikia? Aidha, ni kwani nini inashindwa kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na wakati huo huo inafanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge kutekeleza shughuli ambazo hazipo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo?

## 9. MWENENDO WA HALI YA UCHUMI WA TAIFA

### 9.1. Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishaeleza kuwa miongoni mwa majukumu msingi ya Wizara ya fedha ni pamoja na jukumu la kusimamia deni la Taifa. Hata hivyo, deni hili limeendelea kuwa kubwa kila mwaka jambo ambalo limekuwa na athari kubwa katika bajeti ya Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hivyo kuathiri uchumi wetu na maisha ya wananchi kwa jumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu tathmini ya nusu mwaka ya mwenendo wa uchumi (Mid-Year Review) katika mwaka wa fedha 2017/18 iliyotolewa mwezi Februari, 2018 ni

kwamba; deni la taifa liliongezeka kwa dola za kimarekani milioni 1,054.6 (sawa na shilingi trilioni 2, bilioni 320 na milioni 120)[9] kutoka dola za kimarekani milioni 19,957.6 (sawa na shilingi **trilioni 43 , bilioni 906 na milioni 720) mwezi Juni 2016;** hadi kufikia dola za kimarekani milioni 21,012.2 (sawa na shilingi **trilioni 46 , bilioni 226 na milioni 840) mwisho wa mwezi Desemba, 2017**. Deni hilo linajumuisha deni Serikali la nje na deni la sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,**kwa mujibu wa taarifa hiyo; Deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 8.6 na kufikia shilingi 12,810,300,000,000/= **(trilioni 12, bilioni 810, na milioni 300)**. Kwa hiyo, ukijumlisha deni la nje na la ndani utapata jumla ya deni la taifa kuwa ni **shilingi 59,037,140,000,000/= (trilioni 59, bilioni 37, na milioni 140)**

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa inayoelezwa ya kuongezeka kwa deni ni mikopo mipya pamoja na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha (exchange rate fluctuations). Katika nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ya 2017/18, Serikali ilikopa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 556.0 (sawa na shilingi trilioni 1, bilioni 223, na milioni 200) ambapo kati ya fedha hizo dola za kimarekani milioni 471.1 (sawa na shilingi trilioni 1, bilioni 36

[9] Fedha ya kitanzania imekokotolewa kwa kutumia viwango vya kubadilisha fedha (exchange rate) ya dola ya kimarekani kwa shilingi ya tanzania ambayo kwa sasa ni shilingi 2,200 kwa dola moja ya Marekani.

na milioni 420) zilipokelewa kama fedha taslimu na kiasi kilichobakia cha dola za kimarekani milioni 84.9 (sawa na shilingi bilioni 186 na milioni 780) zilingia kwa mfumo wa ugharamiaji wa moja kwa moja wa miradi ya maendeleo (direct project financing)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho hicho cha nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ya 2017/18; Serikali ililipa kiasi cha dola za kimarekani milioni 453.7 (sawa na shilingi bilioni 998 na milioni 140) kama marejesho ya mkopo wa nje. Kati ya fedha hizo, dola za kimarekani milioni 315.2 (sawa na shilingi bilioni 693 na milioni 440) zilikuwa ni marejesho ya deni msingi (principal repayments) na kiasi kilichobakia cha dola za kimarekani milioni 138.5 (sawa na shilingi bilioni 304 na milioni 700) kilikuwa ni malipo ya riba (interest payments).

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha Serikali kulazimika kulipa riba ya shilingi bilioni 304 na milioni 700 ni matokeo ya kiburi cha Serikali hii ya CCM cha kutotaka kupokea na kuufanyia kazi ushauri wa muda mrefu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa kutochukua mikopo yenye masharti ya kibiashara. Fedha hii tunayolipa kamariba ni fedha ambayo ingetumika kugharamia huduma za jamii kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maangalizo yote ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipatia Serikali hii kuhusu kupunguza kwa kadri iwezekanavyo au kuacha kabisa kuchukua mikopo yenye masharti ya kibiashara; safari hii Serikali imepanga kukopa jumla ya shilingi trilioni 8 bilioni 904, na milioni 727[10] katika mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, ukiangalia sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19 utaona kwamba Serikali imetenga shilingi **trilioni 10, bilioni 4, na milioni 840** kwa ajili ya kulipa deni la taifa.

**Mheshimiwa Spika,** hatua tuliyofikia ya kukopa shilingi trilioni 8 yenye masharti ya kibiashara na kulipa madeni kwa shilinigi trilioni 10 ni mbaya sana. Hii haina tofauti na kuwa kwenye mzunguko wa madeni yasiyoisha (vicious cycle of debts). Tukishakubali kuwa katika mzunguko wa madeni maana yake tuko katika mzunguko wa umasikini pia (viscious cycle of poverty).

**Mheshimiwa Spika,** mikopo ya masharti nafuu ambayo Serikali inatarajia kukopa kwa mawaka wa fedha 2018/19 ni jumla ya shilingi trilioni 2.676. Hiki ni kiasi kidogo na kimeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Tafsiri ya kushuka kwa mikopo yenye masharti nafuu ni kwamba

---

[10] Tazama Jedwali la Sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19

nchi yetu haikidhi vigezo vya kupatiwa mikopo ya masharti nafuu. Na hii ni kwa sababu deni la taifa halijafanyiwa uhakiki (credit rating) ili kujiridhisha Serikali inakopesheka kwa kiwango gani. Kwa sababu hiyo; mashirika mengi ya fedha duniani yamejitoa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa nchi yetu kwa kuwa hakuna uhakika kama mikopo hiyo itaweza kurejeshwa. Matokeo ya jambo hilo, Serikali imekosa namna nyingine ya kumudu gharama za kuendesha nchi, badala yake imekimbilia kwenye mikopo ya masharti ya kibiashara jambo ambalo linaendelea kudidimiza uchumi wan chi.

**Mheshimiwa Spika,** hakuna ubishi kwamba kukua kwa deni la Taifa kunaisababishia serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za kiuchumi za wananchi. Jambo la kusikitisha ni kwamba pamoja na ukweli huo, serikali imeendelea kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara hali ambayo inazidi kufanya hali ya maisha kwa wananchi yaendelee kuwa ngumu kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni hayo badala ya kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishatoa rai kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum (Special Audit) katika

kitengo cha deni la Taifa (Fungu 22) ili tuweze kujua mikopo tunayoichukua kila mwaka inatumika kufanyia nini, atoe taarifa ya miradi iliyotekelezwa kutokana na mikopo hiyo kama ni ya miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa Maendeleo. Halikadhalika ukaguzi huu maalum utatuwezesha kama Taifa kujua kiwango halisi cha deni la Taifa ambalo tunadaiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ilishatoa ushauri kwa Serikali hii kutenganisha deni halisi la Taifa na matumizi mengineyo yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina ili kuziba mianya ya ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kisingizio cha Deni la Taifa. Katika muktadha huo huo, ili kudhibiti Serikali kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara, ambayo hatimaye yanaliingiza taifa kwenye mzigo wa madeni; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza pia kwamba; Kabla Serikali haija kopa; ilete pendekezo la mkopo huo Bungeni pamoja na orodha ya miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mkopo huo ili Bunge liidhinishe. Pendekezo hili lilizingatia msingi kwamba Bunge ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi, na kwa kuwa mikopo hii inakuja kulipwa na wananchi kupitia kodi zao, ni vema wananchi wakashirikishwa kupitia wawakilshi

wao juu ya mikopo ambayo Serikali inachukua kwa niaba ya wananchi.

- **Takwimu Kengeufu za Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017, inaonyesha kwamba kiwango cha deni la taifa kimeshushwa kwa kiasi cha **shilingi 4, 588,390,000,000/= (trilioni 4, bilioni 588, na milioni 390)**

**Mheshimiwa Spika,** CAG anasema kwamba, mapitio yake ya deni la taifa yalibaini kwamba kiwango cha deni la taifa kilifikia **shilingi 46,081,430,000,000/= (trilioni 46, bilioni 81 na milioni 430)** kufikia Juni, 2017; lakini kiwango hicho hakikujumuisha madeni ya **shilingi bilioni 4,588,390,000,000/=,** ikiwa ni madeni ya mifuko ya pensheni kiasi cha **shilingi 4,421,750,000,000[11] na shilingi** 166,640,000,000/= ikiwa ni dhamana zilizokiukwa masharti chini ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** ukichukua kiwango cha deni la taifa kilichoshushwa cha**shilingi 4, 588,390,000,000/=;** ukajumlisha na kiwango cha jumla ya deni la taifa cha

---

[11] Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG kuhusu Ukaguzi wa Fedha za Serikali Kuu ya Machi, 2018; Shilingi 4,421,750,000,000/= ni sawa na asilimia 4.14 ya Pato la Taifa ambalo kwa sasa ni shilingi 106,867,000,000,000/= ( trilioni 106 na bilioni 867).

**shilingi 59,037,140,000,000/=** kilichotolewa na BOT, utakuta kwamba jumla ya deni la Taifa ni **shilingi 63,625,530,000,000/= (trilioni 63, bilioni 625, na milioni 530).**

**Mheshimiwa Spika,** ukirejea hotuba ya Waziri Mkuu aliyoitoa hapa Bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2018/19; tarehe 4 Aprili, 2018; alisema kuwa deni la Taifa hadi kufikia Desemba, 2017 lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 25,419.6[12]. Ukibadili dola hizi kuwa shilingi za Tanzania kwa*'exchange rate'* ya shilingi 2,200/= kwa dola moja ya Marekani utapata jumla ya **shilingi 55,923, 120,000,000/= (trilioni 55, bilioni 923, na milioni 120).**

**Mheshimiwa Spika,** kiwango hiki cha deni la taifa cha takriban shilingi trilioni 63 ni sawa na asilimia 59.43 ya Pato la Taifa ambalo kwa sasa ni shilingi trilioni 106.867 kwa mujibu wa taarifa ya CAG.

**Mheshimiwa Spika,** kuna mkanganyiko kuhusu uhimilivu wa deni la taifa dhidi ya pato la taifa. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha ni kwamba pato la taifa kwa sasa ni shilingi trilioni 50.5 Na kwa mujibu wa hotuba hiyo;

---

[12] Tazama Hotuba ya Waziri Mkuu akiwasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi katika Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2018/19 uk.9 aya ya 16.

uhimilivu wa deni kwa sasa ni asilimia 34 ya pato la taifa wakati ukomo wa uhimilivu ni asilimia 56 ya Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**kwa kutumia takwimu za uchambuzi wa deni la taifa uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni – ambapo deni la taifa limefikia shilingi trilioni 63; ni kwamba deni la taifa si himilivu tena. Takwimu zinazotolewa na Serikali haziwezi kuaminika tena kwa kuwa Serikali hiyo hiyo ina takwimu tofauti kuhusu deni la taifa; na pia kuhusu pato la taifa.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Waziri wa fedha, anasema kuwa pato la taifa ni shilingi trilioni 50.5; taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge inaonyesha kuwa pato la taifa ni shilingi trilioni 86. Wakati huo huo, CAG anasema kuwa pato la taifa kwa sasa ni shilingi trilioni 106. Katika Mazingira hayo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata mashaka juu usahihi wa deni la taifa na pia pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika;** pamoja na ukengeufu huo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashukuru kwa Serikali kujiumbua yenyewe kwamba deni la taifa si himilivu tena kwa kutumia kigezo cha deni dhidi ya pato la taifa. Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu hali ya uchumi ukurasa wa 9 aya ya 16 inasema kwamba; "Pato halisi la

taifa kwa mwaka 2017, lilifikia shilingi milioni 50,525,087 (trilioni 50.5). Kwa hiyo, ukilinganisha na deni la taifa ambalo kwa sasa ni shilingi trilioni 63 ni wazi kwamba nchi iko rehani.

**Mheshimiwa Spika,** kuwa deni la taifa limefikia zaidi ya nusu ya pato la taifa; na ukomo wa kukopa ni asilimia 50 ya pato la Taifa ambayo tumeshaivuka kwa mujibu wa takwimu alizotoa Waziri Mkuu. Hivyo kuendelea kusema kuwa deni ni himilivu ni kujivika kilemba cha ukoka, na kujitoa ufahamu, mambo ambayo hayakubaliki katika kanuni za uchumi. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalisihi Bunge kuazimia kuunda Kamati Teule kuchunguza uhalisia wa deni la Taifa na Pato la Taifa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kushikilia msimamo wake wa kuitaka Serikali kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi maalumu (Special Audit) ya mwenendo wa deni la taifa na kushauri hatua za kuchukua ili taifa liepukane na athari za deni hilo katika uchumi wan chi.

**Mheshimiwa Spika,** Ujasiri wa kusema deni letu ni himilivu, lazima uendane sambamba na uwezo wetu wa kiuchumi wa kukusanya KODI. Deni linaweza kuwa himilivu kama uwezo wa nchi kukusanya kodi unafikia japo 36% ya Pato

la Taifa. Kwa mantiki hiyo,kwa pato letu la Taifa la shilingi Trillion 125, tulitakiwa kwa mwaka tuwe tunakusanya kodi isiyopungua shilingi Trillion 45 kwa mwaka. Kwa makusanyo haya tutakuwa na uwezo wa kulipa deni ,mishahara kwa watumishi wetu na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa hali ilivyo sasa uwezo wetu wa kukusanya ni 14% tu ya pato la Taifa. Taarifa ya Wizara ya Fedha kwa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti inaonyesha kwamba Kati ya shilingi Trillion 17.3 zilizopangwa kukusanywa na TRA katika mwaka wa fedha 2017/18. Mpaka Mwezi Machi 2018 kiasi kilichokusanywa ni shilingi trillion 10.7 tu. Kwa "makusanyo ya Trillion 1.3 kwa mwezi kama tunavyoambiwa na TRA" inatarajiwa mpaka mwaka wa fedha unaisha makusanyo ya Kodi yatafikia shilingi Trillion 14tu!

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na**uwezo mdogo** wa kukusanya mapato unaokwenda sambamba na **mzigo mkubwa** wa deni la Taifa. Utekelezaji wa Bajeti unadhihirisha hilo kwani ¾ ya fedha inayokusanywa inakwenda kwenye kulipa deni la Taifa na Mishahara kwa watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa uchambuzi huu utaona kwamba kuna tofauti ya takwimu za deni la taifa zilizotolewa na Benki Kuu; zilizokaguliwa na CAG na zilizotolewa na Waziri

Mkuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni takwimu zipi sahihi kati ya hizo?

**Mheshimiwa Spika,** ukengeufu huu wa takwimu unatokana na udhaifu uliopo katika mfumo mzima wa usimamizi wa deni la taifa. Mfumo huo, umepitwa na wakati. Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 uliandaliwa kwa mazingira ya sheria ya Mikopo ya serikali , Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (Miaka 43 iliyopita). Hali ya uchumi na mazingira ya kuanzishwa kwa sheria na mkakati wa NDS yamebadilika mno kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kupanuka kwa wigo wa deni la Taifa katika suala la vipengele na mikopo mikubwa ambayo imefanyika, sheria na miongozo inayosimamia deni la Taifa haiko sambamba na maendeleo hayo na vyombo vinavyotumika vimepitwa na wakati na kwa sababu hiyo kufanya usimamizi wa deni la taifa kuwa changamoto.

**Mheshimiwa Spika,** Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali anabainisha [13] katika ripoti yake ya Machi, 2017 kwamba:

---

[13] Ripoti kuu ya mwaka ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali, kuhusu taarifa za fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka unaoishia Tarehe 30 Juni ,2016. Machi 2017, uk.76

**mfumo uliopo sasa unaongeza uzembe katika uendeshaji,uratibu duni na kutokuwa na taarifa za kutosha katika vitengo na taarifa sahihi kupitia taasisi na kusababisha kuwa na rekodi zisizosahihi** na zisizojitosheleza kuhusiana na deni. Alishauri mfumo mzima wa usimamizi wa deni la taifa ufanyiwe maboresho (reform); ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyopo sasa; na hivyo kuweza kuwa na usimamizi mzuri (management) ya deni la taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza; maboresho hayo yaliyopendekezwa na CAG yalishafanyika?

### 9.2. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwamba Pato la Taifa kwa kutumia kizio cha 2015 kwa mwaka 2017 lilikuwa ni shilingi milioni 125,624,406 na pato la taifa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2018 lilikua kwa asilimia 8.4 sawa na shilingi milioni 136,176,856.1. Shughuli za kiuchumi zilizochangia ukuaji huo ni; Ujenzi 28.2%; Kilimo(mazao,mifugo,uvuvi na misitu) 23.1%; utawala na ulinzi 7.4% na usafirishaji na uhifadhi mizigo 7.3% . Lakini katika kipindi hicho shughulizi za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni ujenzi 20% habari na mawasiliano 18.3%, utawala na ulinzi 15.5%, Kilimo 7.1%. Wakati huo huo shughuli za kiuchumi zenye mchango mkubwa kwenye

Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ni Kilimo 31.4% na Ujenzi 13.9%

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa uwekezaji kwenye sekta husika una uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa sekta husika, lakini mchango wa sekta kwenye pato la Taifa una uhusiano wa moja kwa moja na idadi ya watu wanaojihusisha na sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** ukiangalia mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi inaonesha kuwa sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli binafsi 22.8%; shughuli za biashara 20.5%; shughuli za **uzalishaji viwandani 11.1% na kilimo 6.9%.** Hii maana yake ni kuwa Tanzania haiwezi kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati kutokana na ukweli kuwa uwekezaji unaofanyika kwenye maeneo muhimu ya kutupeleka kwenye uchumi huo hawapewi kipaumbele cha uwekezaji. Rejea Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 Uk.8

### 9.3. Mwenendo wa Bei Nchini

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya mpango aya ya 2.2.3.3 unaonesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018 mwenendo wa mfumuko wa bei umebakia katika wigo wa tarakimu moja. Katika mwezi Januari ulikuwa silimia 4.0, Juni 3.4% na Agosti 3.3%. Wakati huo bei za vyakula mfumuko ulipungua kutoka 6.7% hadi 3.2%. Aidha kwa upande wa bei za nishati uliongezeka kutoka 10.4% hadi 18.7% kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi ni kwa vipi bei za mafuta zinapanda wakati huo huo bei za vyakula zinashuka. Kwa kawaida vyakula vingi vinazalishwa maeneo ya vijijini, na inalazimu kuingia gharama za usafirishaji hadi sokoni. Kwa kutumia "Marketing equation" za kupanga bei kwenye soko, jambo hili la mafuta yako juu sana na bei za bidhaa zinazoletwa sokoni ziko chini.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa Serikali inaficha ukweli kwamba uwezo wa wananchi kufanya manunuzi umepungua sana (Purchasing power) kutokana na ukweli kuwa Serikali iliondoa fedha kwenye mzunguko, na pia fedha nyingi zinatolewa kwa makampuni ya nje yanayojenga, na pia athari za vyeti feki kwa wananchi pamoja na makampuni kupunguza wafanyakazi na hivyo kupelekea mzunguko wa fedha kuwa haba. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kutoa tamko kuhusu mzunguko mdogo wa fedha ambao umewafanya wananchi kushindwa kununua bidhaa na inachukua hatua gani kurudisha mzunguko wa fedha katika viwango vinavyokubalika.

### 9.4. Sekta ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kuwa uchumi hauwezi kuimarika kama sekta ya fedha inashuka kiutendaji, Takwimu za mwenendo wa sekta ya benki kwenye Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango aya ya 2.2.3.6 (a) inaonesha ujazi wa fedha kwenye Mabenki umeongezeka kwa wastani wa asilimia 7.0 na kufikia shilingi bilioni 25.2945 mwaka 2017/18 kutokana na kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na

kuimarika kwa sekta binafsi na rasilimali za kigeni katika benki za Biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili halina uhalisia kwani katika kipindi husika imeshuhudiwa mabenki mengi yanafungwa na kupelekea wananchi kupoteza akiba zao, Mfano ni kufungwa kwa Benki ya Wanawake, Benki ya Twiga, na mabenki ya wananchi (Community banks) katika maeneo mbalimbali hapa nchi. Aidha, uimara wa sekta ya benki kwa kuwa na ukwasi wa kutosha ni kutokana na ukweli kwamba zinashindwa kutoa mikopo kwa kuogopa kutokea kwa mikopo isiyolipika na hivyo kupelekea kuweka masharti magumu sana kwa wakopaji.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umefikia asilimia 4 mwezi Juni 2018 ukilinganishwa na asilimia 1.3 mwezi Juni 2017. Sehemu kubwa ya mikopo ikiwa ni ya shughuli binafsi 22.8%(Shughuli zisizoza uzalishaji), na shughuli za uzalishaji viwandani na kilimo mikopo ilikuwa ni kwa 11.1% na 6.9% kwa mfuatano. Shughuli za biashara zilikuwa ni 20.5%, uhalisia hapa ndipo kwenye watu wengi sana lakini asilimia hiyo haiendani na uhalisia wa wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,** hii maana yake ni kwamba bado sekta ya benki haijakuwa imara kuendesha uchumi wetu au hali halisi ya biashara ni ngumu kiasi kwamba benki zinashindwa kutoa mikopo kutokana na uwezekano wa kuongezeka kwa mikopo chechefu (NON PERFOMING LOANS) na hivyo kulazimika kuweka vigezo/masharti ya mikopo kuwa magumu kiasi kwamba wafanyabiashara kushindwa kuyatimiza, Katika Ukurasa wa 9 wa Kitabu